# SHIRIKISHO LA JUMUIYA ZA WANAFUNZI WATANZANIA NCHINI CHINA

# TASAFIC

TOLEO NO.001

01/ 07/ 2019



*Pichani Ni Waziri Mkuu Wa Serikali Ya Jamuhuri Ya Muungano Wa Tanzania Mh.kassim Majaliwa Akiwa Pmaoja Aliyekuwa Waziri Wa Mambo Ya Nje Na Ushirikiano Wa Afrika Mashariki Dr. Augustine Philip Mahiga, Balozi Wa Tanzania Nchini China Mh. Mbelwa Kairuki, Mwenyekiti Wa Tasafic Ndugu Denis Mukama Na Baadhi Ya Mawaziri Kutoka Serikali Ya Mapinduzi Zanzibar, Wafanyabiashara Na Baadhi Ya Watanzania Wanaoishi Katika Jamhuri Ya Watu Wa China. Baada Ya Mkutano Wa Waziri Mkuu Na Watanzania Wanaoishi Au Kusoma Nchini China.*

## MUNGU IBARIKI TANZANIA

## KAULI YA SHIRIKISHO

"Elimu na Umoja Tuijenge Tanzania"

Email: tasafic@yahoo.com Tell: +8615652631291 Facebook: Tasafic China Instagram: tasafic

Ijuwe Tasafic....................................................................................................................................1

Neno La Balozi Wa Tanzania Nchini China ........................................................2

Hivi Ndivyo Ninavyoweza Kuuelezea Uongozi Wa Tasafic 2018/19................3-4

Nguvu Ya Mwanamke.............................................................................................5-6

Elimu Katika Shule Za Msingi Na Sekondari China..........................................7-8

Tanzania Ndani Ya China..........................................................................................8

Fani Za Sayansi, Teknolojia, Uhandisi, Na Hisabati Chachu Ya Maendeleo Endelevu...........................................................................................................9-10

Happy Birthday Tasafic 2019/20...........................................................................11

Je Tunajifunza Nini Kwenye "Internationalization Policy"? ........................12-13

Nilidhani Elimu Ya Tanzania Hainitoshi............................................................14

Miraji Aitangaza Vyema Tanzania Kimataifa.....................................................15

Uongozi Wa Tasafic ...............................................................................................16

Picha Za Wandishi Wa Jarida................................................................................17

# IJUWE TASAFIC

Shirikisho la jumuiya za wanafunzi watanzania katika Jamhuri ya watu wa china ni Chombo kinachowaunganisha Wanafunzi wote watanzania Wanaosoma kwenye taasisi za Elimu katika jamhuri ya watu Wa china kupitia jumuiya zao Zilizopo kwenye majimbo.

Shabaha ya kuundwa Kwa shirikisho hili ni kwa ajili Ya kushiriki kutatua changamoto Za kielimu za wanavyuo na Kuwaandaa kuwa wasomi wenye Kuwajibika ipasavyo na kuwa raia Wema wa taifa letu na kwamba Chombo hiki ni sawa na tanuri la Chuma la kuokea wasomi wazuri Na bora wenye kujitambua. Kwa Hivyo shirikisho la wanafunzi Watanzania wanaosoma katika Taasisi za elimu katika jamhuri ya Watu wa china tunatambua kuwa Kuunganisha ĕ kra za pamoja za Wasomi kutachochea harakati za Kuleta mapinduzi ya kiuchumi, Kisayansi na kitekinolojia na Kujenga jamii ya watu iliyo sawa Nchini tanzania kwa kutumia Elimu na maarifa tunayoyapata.

Ilikufanikishahaya Tunahitaji chombo madhubuti Kinachounganisha fikra na vitendo vya wanafunzi waliopo katika jamhuri ya watu wa china. Shirikisho la wanafunzi Watanzania wanaosoma katika taasisi za elimu katika jamhuri ya watu wa china litatekeleza malengo na madhumuni yake kupitia utaratibu mahsusi Lililojiwekea kwa misingi ya Udugu, usawa, uwajibikaji Na ushirikishwaji katika Kushiriki kikamilifu kusaidiana Kuijenga na kuitangaza nchi yetu Na rasilimali zake kupitia fursa Ya elimu tunayoipata. Shirikisho La wanafunzi watanzania Wanaosoma katika taasisi za elimu katika jamhuri ya watu wa china tutaratibu na kukuza uhusiano na ushirikiano baina yake na taasisi zinazojishughulisha na elimu, sayansi, utamaduni na ajira Katika jamhuri ya watu wa china Na tanzania.

Pia tunazingatia kwamba Elimu ndiyo rasilimali kuu Ya taifa letu, pia tunakubali Kimsingi kwamba ili tuweze Kupata elimu bora wanafunzi Tunalazimika kuwa na nidhamu Na hulka ya uchunguzaji ili kupata Uelewa mpana wenye kuyafahamu mazingira tuliyopo.

Ni imani yetu kwamba Kutokana na misingi mizuri Iliyowekwa katika taifa letu Wanafunzi wote waliopo Nchini China watakuwa mstari Wa mbele kuhakikisha kuwa Tasafic inazidi kukuwa na kutekeleza malengo yake iliyojiwekea na pia kutoa mwanga kwa wanafunzi wengine wa tanzania wapo katika nchi mbali mbali kuona umuhimu wa kutengeneza jumuiya zao kwa lengo la kukuza umoja na mshikamao wa watanzania ambao wapo nje ya nchi.


**Bodi ya Wahariri**

**Mhariri Mkuu**
Mngereza Mzee Miraji

**Waandishi**
Wilson Anatory Bilihanyuma
Phelisters Wegesa.
Fatma Rembo

**Msanifu**
Mohamed Mbaraka Shaali


## UTAMBULISHO

Wapenzi Wasomaji Wa Jarida Maalum La Shirikisho La Jumuiya Za Wanafunzi Watanzania Katika Jamhuri Ya Watu Wa China, Tunayo Furaha Kuwakaribisha Katika Uendelezaji Wa Juhudi Za Umoja Wa Wanafunzi Wanaosoma China. Lengo La Jarida Hili Ni Kukuza Mawasiliano Na Watanzania Kwa Kutumia Njia Tofauti Kama Vile Jarida, Vipeperushi Pamoja Na Vyombo Vingine Vya Habari. Tunakaribisha Maoni Yenu Ili Tuweze Kufikia Lengo Letu Kwa Maslahi Mapana Ya TANZANIA .


Tanzania Students Associations Federation in China c/o.
Tanzania Embassy in Beijing 8 LiangMa He Nan Lu, Sanlitun, 100600 Beijing,
P.R. CHINA
Email: tasafic@yahoo.com

## NENO LA BALOZI



Mh, Mbelwa Kairuki
Balozi Wa Tanzania Nchini China.

Ndugu wasomaji wote wa Jarida hili la TASAFIC.

Napenda kutoa salamu zangu za pongezi kwa uongozi wa shirikisho la wanafunzi China (TASAFIC) 2018/2019 kwa kuweza kuanzisha jarida hili. Hili Ni miongoni mwa ushahidi kuwa Tanzania tumejaliwa vipawa mbalimbali vya uongozi, uandishi hata ubunifu.

Jarida hili ni chapisho la kwanza, ni imani yangu kuwa litakuwa ni chachu ya kulitangaza shirikisho lenyewe na nchi yetu ya Tanzania kwa ujumla.

Maudhui yaliyomo ndani ya jarida hili kupitia mada mabalimbali, yanatupa mwanga wa namna bora ya kukabiliana na changamoto za kimaisha pamoja na kusisitiza uzalendo kwa nchi yetu ya Tanzania. Asanteni sana.

MUNGU IBARIKI TANZANIA.

## MADHUMUNI NA MAJUKUMU YA TASAFIC

a) Kuwapokea na kuwaongoza wanafunzi wa kitanzania wanaofika nchini China kwa mara ya kwanza.

b)Kuwaunganisha wanafunzi Watanzania wanaosoma na kuishi katika Jamhuri ya watu wa China.

c) Kushughulikia uratibu wa masuala ya kielimu ya Wanafunzi kupitia vyama vyao vilivyopo majimboni.

d) Kuwa kiungo kati ya Wanafunzi na Ubalozi.

e)Kusimamia na kushirikiana na jumuiya wanachama katika shughuli mbalimbali za kijamii zinazowahusu wanajumuiya.

f) Kusambaza taarifa za fursa mbalimbali kwa watanzania wote ikiwa ni pamoja na ufadhili wa masomo na ajira nchini Tanzania na China.

g) Kuwa kiungo kwa serikali za Tanzania na China kwa kupitia Ubalozi na Wanafunzi waishio katika Jamhuri ya watu wa China.

h) Kuwasilisha na kutetea maslahi na haki za wanafunzi wa kitanzania walioko masomoni katika Jamhuri ya watu wa China.

i) Kushiriki kikamilifu katika fursa zenye kuweza kuitangaza nchi yetu na rasilimali zake katika Jamhuri ya watu wa China.

j) Kushiriki katika mikutano, midahalo na makongamano ili kuwajengea wanajumuiya uwezo katika masomo yao.

k)Kuwajenga wanajumuiya katika maadili ya uzalendo, umoja na utaifa.

l) Kushuirikiana na Ubalozi wa Tanzania uliopo Jamhuri ya watu wa China kuwatafutia wanafunzi mafunzo ya muda mfupi na mazoezi ya vitendo ili kukuza kiwango chao cha elimu na kuwajengea uwezo zaidi

m) Kuwa chemchem ya fikra na mawazo ya kimaendeleo kwa Taifa.

n)Kufanya tafiti za changamoto zinazolikabili Taifa.

o) Kushirikiana na watanzania waliowahi kusoma katika Jamhuri ya watu wa China kutengeneza fursa zaidi za kielimu na ushauri kwa Serikali ya Tanzania.

p)Kushirikiana na ubalozi kuwaunganisha wanashirikisho na watanzania kwa ujumla na viongozi kutoka serikalini, asasi za kiraia, mashirika, makampuni na wageni mbalimbali wanaotembelea Jamhuri ya watu wa China.




*Viongozi wa TASAFIC pamoja na baadhi ya viongozi wa jumuia mbalimbali walipokutana katika mkutano wa waziri mkuu na watanzania waishio na kusoma China. Kutoka kushoto ni Bi Victoria Makamo Mwenyekiti wa TASAFIC, Bw. Gamba Mwenyekiti wa jumuia ya Beijing, Bi.Phelister Mwenyekiti jumuia ya Henan, Bw. Mukama Mwenyekiti TASAFIC, Bi. Lucynancy mweka hazina TASAFIC na Bw. Yazidi Mwenyekiti jumuia ya Chingdao*

Na:Wilson Anatory Bilihanyuma

Kutokana na hulka yangu ya kupenda kufuatilia matendo/maamuzi, kauli na misimamo ya viongozi wa aina zote, huwa ninabahatika kujifunza mambo mengi sana kwa watu hao walioshikilia hatima ya taasisi wanazoziongoza. Kwa nafasi yangu ya uwakilishi wa jumuiya ya Jilin nimeweza kufanya kazi kwa ukaribu na viongozi wa ngazi za juu wa TASAFIC 2018/19. Kama leo mtu angeniuliza ni namna gani naweza kuuzungumzia uongozi wa juu wa TASAFIC unaomaliza muda wake, ningeweza kunena yafuatayo;-

Kwanza ninapenda kuwapongeza kwa kupata fursa hiyo ya kuongoza shirikisho la wasomi. Ni nafasi ambayo ukiichunguza kwa umakini, utagundua si nyepesi kwa kila mtu. Kwa lugha rahisi, hawa walikuwa viongozi wanaoongoza viongozi wenzao. Ni jambo dogo hili? Ilihitajika busara kubwa kwakuwa unaowaongoza huenda wana uwezo kuliko hata wewe. Kwa kusimamia nafasi hiyo bila kute tereka mpaka leo ninawapongeza sana.Bila kukuchosha, najielekeza kwenye mambo makuu niliyojifunza na ambayo yananifanya niwapongeze leo;

Kwanza kabisa Kulitangaza Shirikisho ndani na nje ya China. Ni wazi kwamba Juhudi kubwa sana zimefanyika kuifanya TASAFIC ifahamike ndani na nje ya China.

Sidhani kama kuna mwanafunzi aliyeko China haifahamu TASFIC. Wengine wameifahamu tangu walipoanza kufikiria kuja China. Mara kadhaa nimelisikia neno TASAFIC katika vyombo vya habari vya Tanzania. Tumepata viongozi wa kitaifa ambao walitembelea China wakaitambua TASAFIC na kuongea na wanachama wake. Si hilo tu, Kuna makundi mengi sana ya "Whatssap" yalianzishwa kuwakutanisha wanafunzi wa kila kada kwa lengo la kufahamiana na kusaidiana. Ukienda "instagram" na "twitter" kote utaikuta TASAFIC na inafanya vyema sana katika kujitangaza. Uendeshaji wa makundi yote haya unaratibiwa na viongozi wa TASAFIC.

Pili,Umakini katika Mawasiliano nje na ndani ya China. Katika hali iliyoelezwa hapo juu ya kujitangaza kwa namna mbalimbali, endapo uongozi usingekuwa makini tungekuwa tumeshaleta mkanganyiko wa taarifa kwa jamii ndani na nje ya China. Hata vyombo vya habari vyenye waandishi waliobobea huwa kuna wakati wanakosea utoaji wa taarifa na kuomba radhi au kupigwa faini. Hili halijawahi kujitokeza TASAFIC kutokana na umakini wa mawasiliano uliopo.

TASAFIC chini ya viongozi waliopo iliwahi kuwatangazia wanafunzi na hata kuwasaidia katika kuomba nafasi za masomo China. Wengi tulidhani kwamba hili lingeleta taswira mbaya kama matapeli wangejipenyeza katikati na kuibia watu kupitia jina la TASAFIC. lakini kutokana na umakini wa viongozi wetu jambo hili lilifanyika kwa ufanisi mkubwa bila tatizo lolote la kiuharifu. Viongozi wao wenyewe wameonesha kuwa na mawasiliano ya karibu. Hili linathibitishwa na kwamba, hawajawahi kupingana katika taarifa wanazotoa kwa wanachama. Aidha, hakuna barua waliyotoa na kuleta mkanganyiko wowote au kuibua maswali mengi yasiyojibika. Katika hili wamefanikiwa sana.

Tatu,Kuimarisha umoja na mahusiano ya wanafunzi na wadau wengine. Kwa mtu anayekumbuka vyema, uongozi huu ulianza awamu yake katika mazingira ambayo hayakuwa shwari. Baadhi ya watu walikuwa wamegawanyika na

**UK,4**

kuonesha kutoridhika na uchaguzi. Hii ilitokana na mvutano uliokuwepo kwenye kipengele mojawapo cha katiba walichotaka kibadilishwe kabla ya uchaguzi kufanyika, jambo ambalo halikufanyika. Kutokana na hilo, ushirikiano ulikuwa mdogo sana kwa uongozi na hii ilileta wasiwasi kwamba huenda ingekuwa mwisho wa TASAFIC. Busara za viongozi hawa ndizo zilizowavuta mtu mmoja mmoja na hata kufikia muungano imara tulionao leo. Ninakosaje kuwapongeza kwa mfano!. Kuna siri kubwa sana iliyowafanikisha katika hili ambayo imeelezwa katika kipengele namba tano.

Nne,Utayari wa kuhudumia wanachama. Katika uzoefu wangu wa kufuatilia viongozi niligundua viongozi wa aina mbili. Wapo wanaoingia madarakani kwasababu wanapenda kuitwa kwa cheo kile anachokishikilia. Msukumo mkuu kwa viongozi wa aina hii ni kupata heshima ya cheo kile na sio kitu kingine; suala la kuwahudumia watu ni chaguo la pili au la tatu kwao. Viongozi wa aina ya pili ni wale wanaoingia madarakani kwa sababu wanapenda kuhudumia watu. Hawa wanaumizwa na shida za watu na furaha yao huja mwisho baada ya kuona walio chini yao wamefurahi.

Uongozi wa TASAFIC 2018/19 ni uongozi uliopenda kujitoa katika kuhudumia watu. Sisi wanachama tumewasumbua sana kuliko wao walivyotusumbua sisi. Kuna michango ya matibabu na maafa walichangisha, wameratibu maboresho ya kanuni mbalimbali za TASAFIC, wameratibu ujio wa wanafunzi wapya China, wameratibu na kutushirikisha fursa mbalimbali za ajira, masomo, mikutano, makongamano nk. Ikumbukwe hakuna masilahi yoyote wanayolipwa. Ni moyo wa kujitoa uliotawala.

Katika kuhakikisha huduma zinakuwa za uhakika, hawakupenda kufanya kila jambo wao wenyewe. Walishirikisha watu au kuunda kamati mbalimbali. Mfano waliunda kamati ya mabadiliko ya katiba, Tume ya uchaguzi, Uandishi wa Makala za TASAFIC nk. Mgawanyo wa majukumu 'Delegation of power' ni nguzo kuu ya mafanikio katika uongozi wowote. Kiongozi huwezi kufanya kila kitu peke yako bila kuwaamini watu na kuwashirikisha. Katika hili, nawapongeza sana.

Uongozi umeiunganisha vyema TASAFIC pamoja na mlezi wetu ambaye ni Balozi wa Tanzania nchini China. Sasa tunapata taarifa nyingi zinazotuhusu kutoka ubalozi kupitia kwa viongozi wetu. Mfano, upatikanaji wa "Passport" mpya za kusafiria katika ubalozi wetu China.

Tano, Kudhibiti hisia binafsi. Hapa ndipo wengi wanaposhindwa uongozi. Kuna ukweli kwamba unapofanya au kusema jambo lolote katika watu wengi, kila mtu anaweza kutengeneza maana tofauti kutokana na elimu, fikra au uzoefu wake. Jambo hili ni maradufu kwa wasomi wanaochambua mambo kwa mitazamo mbalimbali. Jamii yetu ya TASAFIC ina watu wanaoamini katika itikadi tofauti za dini, siasa, kabila, falsafa nk. Viongozi nao wana itikadi zao kama watu wengine ambazo zisipodhibitiwa itakuwa ni vurugu tupu. Kwa masilahi ya TASAFIC, viongozi wetu waliweza kuficha au kudhibiti hisia zao zote kulinda ustawi wa shirikisho. Nawapongeza sana katika hilo.

Katika hali ambayo kila mtu ni kama anajua, hakuna siku ambayo kiongozi wa juu alionesha kughadhabika, kutoa lugha mbaya, kudharirisha, kumkandamiza au kumnyanyasa mtu yeyote hadharani. Wameendelea kuwa wanyenyekevu na kutumia lugha nzuri kwa kudhibiti hisia zao. Hongereni sana.
Jambo moja tu ambalo sikulipenda kwa uongozi huu ni tabia ya kuchelewa au kukaa kimya kabisa pasipo na ulazima wa kufanya hivyo, katika baadhi ya mambo. Ninatambua ukweli kwamba, kukaa kimya ni njia mojawapo ya kutatua au kuzuia tatizo lakini njia hii si wakati wote itafanya kazi.


Kuna wakati ukikaa kimya unaweza kuongeza ukubwa wa tatizo badala ya kulitatua. Labda kutokana na hofu ya matokeo ya utendaji wao, kuna wakati walikuwa wanakaa kimya kwa kitu ambacho kilihitaji ufafanuzi au utendaji wao. Aidha kuna baadhi ya mambo waliishia kuyawasilisha kwa wanachama lakini hawakuleta mrejesho wa hatima ya mambo hayo. Mfano, miezi kadhaa iliyopita waliwahi kuleta hoja ya kuandaa Jarida la TASAFIC, baadae walikaa kimya kwa muda mrefu bila kutoa taarifa ya nini kinachoendelea mpaka walipokuja kuibuka na jarida hili lililokamilika.

Viongozi waliwahi kutangaza kuwa kuna mtanzania aliyeonesha nia ya kuwatafutia wanafunzi nafasi za mafunzo ya vitendo, hatukupewa mrejesho kuhusu mtu huyo mpaka uongozi unapomaliza muda wake.
Mwisho, ninawapongeza viongozi wote na wawakilishi wa majimbo yote kwa juhudi zenu za kuendelea kuwaunganisha watanzania walioko China na kudumisha ushirikiano miongoni mwao. Kwakuwa wazazi wetu tumewaacha nyumbani, hatuna budi kuleana sisi wenyewe na kwa msaada wa Balozi wetu wa Tanzania nchini China ambaye pia ni mlezi wa TASAFIC. Nimeyaandika haya ili Viongozi wajao, wajifunze yale mazuri yaliyofanywa na viongozi wanaomaliza muda wao na watambue kabisa kwamba sisi tunaoongozwa tunafuatilia utendaji wao. Kama tunavyoweza kukosoa mambo mabaya, hatutasita kupongeza mambo mazuri yanapotendeka. Mungu ibariki TASAFIC, Mungu ibariki Tanzania na Watanzania.

**Ukikubali Wajibu, Timiza Wajibu!**

*Wilson Anatory Bilihanyuma*
*Northeast Normal University*
*Jumuiya ya TASAJI – Jilin*
*wilsonanatory@gmail.com*

# NGUVU YA MWANAMKE



*Fatma Rembo Mwanafunzi Wa Shahada Ya Uzamili Katika Fani Ya Sayansi Ya Kompyuta Na Teknolojia (uhandisi wa programu) Akiwa Ndani ya Maabara Ya Komputa Katika Chuo Cha Wenzhou University, Wenzhou, Zhejiang, China.*

Na : Fatma Rembo

**S**habaha ya Makala hii ni kumkumbusha mwanamke nguvu aliyonayo kuleta maendeleo katika taifa lake na jinsi safari moja inavyoweza kubadilisha maisha yake kama akiwa mwenye juhudi, Uthubutu na upambanaji lakini pia kumuhimiza mwanamke kuweza kufikiri kwa usawa,kujenga weledi na uvumbuzi kwa mabadiliko .

Naitwa Fatma Rembo,ni binti wa kitanzania mwenye uzalendo,ujasiri na utayari katika dhana ya kuleta maendeleo. Jitihada, uwajibikaji na uzalendo ndio msingi mkuu wa itikadi yangu na silaha kuu niitumiayo katika kufikia malengo yangu tukufu. Mimi ni mhandisi ila pia binti mwenye kipawa cha uongozi kwani maisha yangu kwa ujumla nimekuwa nikiwa kiongozi katika nyanja tofauti mpaka sasa. Maisha yangu kwa ujumla yamekuwa yakiakisi mtu mwenye busara,upendo na kusaidia watu na kushiriki kwenye mambo ya jamii. Ujasiriamali , ni moja ya kitu nikipendacho na kukifanya kwa ubunifu na weledi mkubwa hivyo kunipa mafanikio lukuki.

Ni Imani yangu kuwa kila binti wa kitanzania anakipaji kimoja au zaidi ambacho akikitumia kwa shabaha ya kuleta maendeleo basi umaskini na kukosa ajira kunakuwa ndoto hivyo kupunguza umaskini kwa kiwango kikubwa ndani ya nchi yetu pendwa Tanzania. Wanawake kama wajasiriamali ,wakulima , wafanyabiashara ,wavumbuzi ni chachu ya kukuza uchumi . Wanawake wakifanikiwa huzalisha na kuongeza athari katika kuwekeza sehemu kubwa ya mapato yao kwa ajili ya ustawi wa familia zao na jamii huku wakijenga faida za muda mrefu kwa kizazi kijacho.

Mnamo mwaka 2016 Octoba nilijiunga na chuo kikuu cha Wenzhou, katika mji wa Wenzhou, jimbo la Zhejiang nchini China katika programu ya Shahada ya uzamili wa sayansi ya kompyuta na teknolojia nikijikita kwenye utaalamu wa uhandisi wa programu. Safari ya masomo yangu imekuwa ya kunijenga, kuniimarisha na kuongeza ujuzi wangu kwa kiwango kikubwa. Chuoni kwangu nilihudumu kama kiongozi Mkuu wa kitengo cha burudani na michezo katika jumuiya ya uongozi ya wanafunzi wa kimataifa kwa mwaka 2017-2018.Lakini pia kwa mwaka 2018/2019 nimehudumu kama Mwenyekiti wa Jumuiya ya Watanzania Wenzhou (Wenzhou Tanzanian Students Association-WETASA) ambazo ni moja kati ya jumuiya zinazounda TASAFIC (Tanzania Students Associations Federation In China) na nimehudumu kama katibu mkuu wa ccm katika shina la Zhejiang nchini China . Nimekuwa miongoni wa wanafunzi wa kiafrika na wa kitanzania Hufaulu kwa kiwango kikubwa na kupelekea kushinda na kuzawadiwa scholarship ya mwanafunzi bora wa kitanzania katika kozi yangu kwa miaka mitatu mfululizo.




*Kutoka Kushoto Ni Victoria Mwanziva Makamu Mwenyekiti Watasafic, Wakatikati Ni Mwenyekiti Denis Mukama Na Kulia Ni Muweka Hazina Lucynancy John .*

Kama hio haitoshi nimekuwa nikichaguliwa kuwa mwakilishi wa pekee wa kike kuwakilisha chuo changu katika semina zinazohusu kozi yangu na programu mbalimbali nchini China .

Sehemu zote hizi sikuwahi kuacha au kusahau utaifa wangu, nimekuwa nikiipeperusha bendera ya Tanzania vyema na kufanya Nchi yangu kupata heshima inayostahiki. Pia imenifundisha kuongeza zaidi kasi ya uchapakazi na uwajibikaji ili kuyafikia malengo yangu.Mbali na yote mimi ni mjasiriamali hivyo nikiwa kwenye maandalizi ya kutimiza ndoto zangu kwa kufanya vitu vikubwa vitakavyoweza kuleta maendeleo ndani ya nchi yangu pendwa Tanzania.

Wanawake wengi wamekuwa ni waoga na kutojiamini hususani kwenye masomo ya sayansi , kwasababu ya mfumo waliozoea kuona na kusikia kuwa masomo hayo na kazi za mfumo huo hufanywa na vijana wa kiume pekee kutokana na ugumu wake. Na hata dunia kuamini zaidi wanaume kuliko wanawake hususani kwenye masuala hayo. Wanawake duniani wanawakilishwa kwa kiwango kidogo sana katika sayansi,teknolojia,uhandisi na hesabu kwenye sekta mbali mbali duniani. UNESCO imeripoti kuwa wanawake wamekuwa wakijiunga kwa kiwango kidogo kwenye masomo hayo huku kiwango hicho kikiwa mawasiliano na teknolojia (3%) ; sayansi asilia ,hesabu na takwimu (5%) huku uhandisi ,ujenzi na viwanda (8%) . Uwiano wa kijinsia katika utafiti wa anga upo chini zaidi. Kwa sasa Africa inashuhudia uhitaji mkubwa wa sekta ya utafiti wa anga, ila bado hakuna alama ya ongezeko la wanawake wanaojiunga kwenye sekta hiyo.

Ni vyema kama wanawake tukajiamini na kufikiri kwa usawa bila kuona kama jinsia ni kikwazo kwenye sekta zote za sayansi ,teknolojia na uhandisi .Wanawake tunauwezo mkubwa wa kujenga kwa weledi pamoja na kuleta mabadiliko. Nawasihi wanawake wote kuweka dhamira na kuwa na uthubutu .Kila penye nia pana njia basi hakika kila jambo linawezekana kikubwa ni kuweka malengo na kujiamini bila kujali jinsia.

Ningependa kuwapongeza wanawake wote wapambanaji katika sekta mbali mbali madaktari, wahandisi, wanasayansi, wafanyabiashara, wanasiasa, wanauchumi, wakulima, wajasiriamali, wanaharakati ,wahasibu,marubani na wafanyakazi wote kwa ujumla katika vitengo vyote. Pongezi hizo zisiwasahau wanawake wote nchini waliowahi na wanaofanya mambo makubwa na kuthubutu kushiriki katika kuleta maendeleo katika taifa letu . Wanawake tunayofasi kubwa ya kuleta maendeleo hivyo tuzidishe kasi ya upambanaji ili tuweze kuleta mabadiliko .

Pongezi kubwa za dhati zimuendee Mwanamke wa kwanza kuwa Makamu wa Raisi nchini Tanzania , Mheshimiwa Samia Hassan Suluhu . hakika umeonesha zaidi kuwa wanawake tunaweza bila kujali jinsia ulithubutu na kuandika historia kuwa mwanamke wa kwanza kushika nafasi hiyo . Nawasihi mabinti wote kusoma shule ,kuzingatia masomo na kujiamini kwani jamii hufanikiwa zaidi mabinti na wanawake wakiwa na elimu pia ni muhimu katika kufikia kiwango kikubwa cha ongezeko la uchumi na maendeleo.Elimu ni haki ya msingi kwa kila binti na kila binti anakipaji,anaweza kukikuza, kukitumia na kuleta maendeleo nchini.

Kwa kumalizia wanawake tusisite kujaribu kila fursa tunayoiona mbele yetu ,ni vizuri kujaribu kuliko kukaa bila kupiga hatua yoyote, tuwe wepesi wa kuchangamkia fursa na kujituma.Kumbuka hakuna aliefanikiwa kwa kukaa tu ila wapo waliofanikiwa kwa kuweka dhana ya uoga pembeni na kuwa na uthubutu .

“KAMA MWANAMKE HAKIKISHA UNAIJUA NGUVU YAKO,HAKIKISHA UNAJIAMINI,UNA WAZO KUBWA LITAKALOWEZA KUBADILISHA MAISHA YAKO NA UNAPAMBANA BILA KUKATA TAMAA , UKIANGUKA NYANYUKA ANZA UPYA ZIDISHA KASI YA MWENDO , FUATA KILE KIGUMU KWANI CHEPESI HAKIKA HAKITOKUFIKISHA MBALI”

• • • • • • • • • • • • • • • •

Fatma Rembo
Wenzhou University
rembofatma@gmail.com



*Mwalimu Wilson Anatory Bilihanyuma akiwa na wanafunzi wa kidato cha pili alipotembelea shule ya sekondari ya 'Changchun 87 Middle School katika ziara ya kimasomo Nchini China.*

Na:Wilson Anatory Bilihanyuma

China ni moja ya nchi zenye idadi kubwa ya wanafunzi pamoja na mfumo mpana wa elimu duniani. Hii ni kutokana na idadi kubwa ya watu wake wanaokadiriwa kuwa zaidi ya 1.3 bilioni. Pamoja na mazingira hayo, China imepiga hatua kubwa sana katika ubora wa elimu inayotolewa kuanzia shule za msingi hadi vyuo vikuu. Nikiwa kama Mwalimu, nilipata fursa ya kutembelea baadhi ya shule za msingi na sekondari za mjini na vijijini ili kujionea hali halisi ya malezi katika shule za China.

Nilishiriki vipindi kadhaa darasani kuona ufundishaji unavyofanyika. Nilienda mbali zaidi kwa kushiriki kikao cha wazazi katika shule mojawapo. Niligundua kwamba, tunafanana katika mambo mengi yanayofanyika shuleni, wanachotuzidi ni ubora katika ufundishaji, pamoja na miundombinu muhimu katika utoaji wa elimu . Kuna mambo mengi ya kujifunza katika kuboresha elimu yetu ya Tanzania. Kwa uchache wake ni kama ifuatavyo;-

Walimu wenye wito na wanaowajibika kitaaluma, mbali na mwonekano wa kujiamini pamoja na lugha ya kitaaluma walimu wanaonekana kuwa wenye utayari wa kusaidia wanafunzi wao. Ni watu wenye ushirikiano na ukarimu kwa wanafunzi wao na hata kwa wageni toka nje ya shule. Adhabu zinazotolewa na walimu, ni zile zinazomfundisha mwanafunzi badala ya kuishia kumuumiza tu. Kwa mfano, mwanafunzi anaweza kupewa adhabu ya kutunga mtihani/ maswali kwaajili ya wanafunzi wengine; kupewa maswali mengi zaidi ya kufanya kuliko wanafunzi wengine nk. Adhabu hizi huweza kumbadilisha mwanafunzi katika njia chanya badala ya viboko
au vitisho vingine vinavyomuharibu mtoto kuliko kumjenga.

Mkazo katika elimu ya uraia na maadili, katika shule zote nilizotembelea, wanafunzi walionekana kuwa na nidhamu, utulivu na wenye kusikiliza. Kupitia somo la maadili, wanafunzi hufundishwa kujiheshimu, kuheshimu wakubwa zao, mamlaka pamoja na Taifa lao. Shule huwa na chumba maalumu cha ushauri nasaha pamoja na michezo ya kusisimua akili kwaajili ya watoto wanaogundulika kuwa na msongo wa mawazo. Katika kila darasa au maeneo mbalimbali ya shule, zinaonekana bendera nyingi kubwa na ndogo za nchi yao. Wanafunzi hupitia mafunzo ya uzalendo jeshini kabla ya kujiunga vyuo vikuu. Kwa msingi huo, elimu ya uraia na maadili inajidhihirisha hata kwa watu wazima wachina. Hali hii imechangia kuimarisha usalama wa raia na kupunguza matukio ya uharifu katika mitaa yote, ambapo unaweza kutembea peke yako hata usiku wa manane bila kudhuriwa na mtu.

Hili ni jambo la kupongezwa na linalostahili kuigwa na
nchi zingine. Bidii ya kazi na shauku kubwa ya mafanikio, wanafunzi wanaonesha bidii kubwa ya kufanya kazi pamoja na uvumilivu kutokana na shauku kubwa ya mafanikio aliyonayo kila mmoja. Hii ni sifa kuu anayoihitaji kila mtu kuwa nayo. Idadi kubwa ya wanafunzi nchini China inapelekea ushindani mkubwa wa fursa za masomo, ajira na fursa zingine, hivyo kumulazimu kila mmoja kusoma kwa bidii kubwa.

Sababu nyingine ni ya kihistoria kutokana na ukweli kwamba, miaka ya nyuma iliyopita kila mzazi alilazimika kuwa na mtoto mmoja tu kama sera ya nchi. Mtoto huyo alijijua kabisa kwamba ndiye pekee anayetegemewa kulea wazazi wake baadae.

Hivyo alilazimika kusoma kwa nguvu zote akiwa na shauku ya kufanikiwa kwaajili ya kuwasaidia wazazi wake watakapozeeka. Inasadikika kuwa, wanafunzi wa China ndio wanaopewa mazoezi mengi zaidi kuliko wale wa nchi zingine zote, ambapo huzifanya wakiwa shuleni na nyumbani. Hii inawapelekea kushikilia nafasi za juu katika mitihani ya upimaji ya kimataifa

**UK,8**

(Program for International Students Assessment, PISA). Kiwango kikubwa cha wanafunzi kujiamini, kinachovutia ni hali ya wanafunzi kujiamini sana kwa kile wanachokijua. Wanapojibu maswali ya mwalimu darasani, wanaongea kwa kujiamini bila hofu na wasiwasi.

Hii ni wazi kwamba Wanafunzi wanachangamka na kuonesha ushindani mzuri darasani. Hakuna mipaka mikubwa sana kati ya walimu na wanafunzi. Wanafunzi wanaonekana kujua vizuri mafanikio na maendeleo ya nchi yao kutokana na simulizi wanazozitoa wanapoulizwa. Kujali afya za wanafunzi, hili ni jambo linalopewa umuhimu wa kipekee shuleni. Hata katika shule za msingi, mwanafunzi haandikishwi bila kupimwa afya kujua kama ana magonjwa hatarishi kwake na kwa wengine.

Mazoezi ya viungo kwa wanafunzi ni kama utamaduni wa kawaida kwaajili ya kuimarisha afya zao. Hii ni sambamba na kuwa na viwanja vizuri vya michezo pamoja na vifaa vya michezo vya aina mbalimbali. Wanafunzi wanapotaka kujiunga na vyuo mbalimbali, hulazimika kupima afya zao upya ili kuwianisha hali ya kiafya na fani anayochagua kusomea. Hili ni jambo zuri kwa manufaa ya mwanafunzi pamoja na serikali kwa ujumla.

Msisitizo kwa kila mwanafunzi kushika nafasi ya kwanza, pamoja na kwamba wanafunzi wanahimizwa kushirikiana, kila mmoja anahimizwa kuwa wa kwanza darasani. Wanafunzi wanafundishwa kwamba, katika maisha ni lazima uwe wa kwanza katika kila kitu unachokifanya. Kila mmoja anahimizwa kutumia ubunifu wake kufanya kitu cha tofauti kuliko mwingine. Wale wanaofanya vizuri hutambuliwa kwa njia mbalimbali kama vile; kuzawadiwa, picha zao au kazi zao (mfano Insha bora) kubandikwa sehemu za wazi nk.

Hii humfanya kila mmoja kufanya kila linalowezekana kuitafuta nafasi ya kwanza darasani. Mwisho, lengo kuu la utoaji wa elimu katika nchi yoyote ni kuleta ukombozi wa fikra na kuandaa rasilimaliwatu inayohitajika kwa jamii na serikali husika. Ubora wa rasilimali hiyo hutegemea ubora wa elimu inayotolewa, ubora wa walimu pamoja na miundombinu.

China imepiga hatua kubwa sana katika kuandaa wataalamu wa kutosha na wenye ubora unaostahili, katika njanja mbalimbali ikiwemo sayansi za uhandishi, usanifu wa majengo, afya, utafiti, utamaduni, anga nk. Karibia nchi zote zinazoendelea duniani, leo zinawatumia wataalamu kutoka China katika ujenzi wa miundombinu yao kama barabara na majengo makubwa. Kupitia njia hii, makampuni ya kichina hunufaika kibiashara huku nchi yao ikiendelea kuimarika kiuchumi.

Ni jambo la kupongezwa kwamba wanajitosheleza kwa wataalamu wanaotumika ndani na nje ya nchi zingine kwa wakati mmoja. Ni wajibu wetu sisi watanzania wachache tunaopata nafasi ya kuja kusoma nchini China, kujifunza mambo mbalimbali yanayoweza kuwa chachu ya mabadiliko katika mifumo ya nchi yetu Tanzani. Kuna wanafunzi wengi wanaosoma kozi mbalimbali nchini China ambao wakitumiwa vyema wanaweza kuongeza tija katika maendeleo ya nchi yetu Tanzania,

*Wilson Anatory Bilihanyuma*
*Northeast Normal University*
*Jumuiya ya TASAJI – Jilin*
*wilsonanatory@gmail.com*

## TANZANIA NDANI YA CHINA

Na : Wilson Anatory Bilihanyuma

Umewahi kukaa chini na kujiuliza maana halisi ya msemo usemao 'Jisikie kama nyumbani'? Wakati fulani niliwahi kutembelea jengo moja lililopo katika mji wa Changchun nchini China. Kitu kimoja kilichonistaajabisha ni kwamba, nilijikuta ghafla nimetokezea nchini Tanzania baada ya kuingia ndani ya jengo hilo lenye ghorofa moja. Swali likanijia kichwani, nimefikaje Tanzania bila kupanda ndege?

Niliporudi nje ya jengo nilijikuta tena niko ndani ya nchi ya China. Hapo nikabaki nimepigwa butwaa. Nikajiuliza, inamaana huku nako kuna uchawi mpaka nakutana na maajabu haya? Baada ya kufikiri na kuulizia vizuri ndipo nikasimuliwa ukweli wa mambo hayo kama ifuatavyo;

Jengo hilo lipo katika mji wa Changchun unaopatikana nchini China upande wa kaskazini mashariki. Ni jengo la makumbusho ya Sanaa za Kimakonde toka Tanzania. Kutokana na kuhifadhi sanaa na vinyago vya kimakonde jengo hilo ni maarufu kwa jina la Makonde Arts. Jengo zima chini hadi juu limepambwa kwa vinyago mbali mbali vinavyotengenezwa na Wamakonde wanaopatikana nchini kwetu Tanzania. Kuta zote zimepambwa kwa picha tofauti tofauti za utamaduni wa Kitanzania. Kwa lugha rahisi ni sawa na kusema 'Tanzania ndani ya China'.

Mara unapoingia ndani ya jengo, utakaribishwa na hotuba zilizoandikwa kwa lugha ya Kiswahili za Rais wa awamu ya tatu na ya nne wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Benjamin W. Mkapa pamoja na Mhe. Jakaya M. Kikwete. Pia kuna picha kubwa ya Rais wa kwanza wa Tanzania Mwl. Julius K. Nyerere. Baada ya kuingia katika jengo hilo unakosaje kujisikia kama uko nyumbani Tanzania?

Kwakuwa tulikuwa katika ziara ya kitalii tukiwa katika kundi kubwa la watu kutoka nchi mbalimbali, Watanzania tuliokuwa wa nne tulijisikia furaha sana kwakuwa kila mtu alianza kutuangalia sisi na kutuuliza maswali mengi kuhusu Tanzania.

Jambo hili ni jema sana kwakuwa ni namna nzuri ya kutangaza vivutio vya utalii vilivyopo nchini kwetu Tanzania, ikizingatiwa kwamba makumbusho hayo yanatembelewa na Maelfu ya watu kutoka nchi mbalimbali.

Pongezi nyingi ziwaendee viongozi wetu wa Serikali waliofanikisha jambo hili kubwa kufanya makubaliano na nchi ya China kwaajili ya kuwa na makumbusho maalumu kwaajili ya sanaa na tamaduni za kabila la Kimakonde, lililojibebea umaarufu wake katika uchongaji wa Vinyago vinavyowakilisha maisha ya mwanadamu wa kiafrika.

*Wilson Anatory Bilihanyuma*
*Northeast Normal University*
*Jumuiya ya TASAJI – Jilin*
*wilsonanatory@gmail.com*



*Aliyesimama katikati ni Phelisters Wegesa Marwa akiwa katika ziara za kimasomo nchini china akipata maelezo kuhusu kuhusu mfumo wa elimu nchini china*

Na : Phelisters Wegesa.

Maendeleo ya China yametoa uzoefu wa mafanikio na matarajio makubwa kwa nchi nyingine ambazo zinahitaji kujikomboa kiuchumi, ikiwakilisha mchango mkubwa kwa Uchumi wa dunia kama mfano wa maendeleo ya uchumi wa kisasa. Uongozi wa nchi ya watu wa China unategemea zaidi tafiti kama nguzo kubwa ya Maendeleo yake kusaidia kubadilisha mwelekeo wa uchumi wa kutoa huduma za msingi, kuweka uvumbuzi na utafiti kwenye mipango yake kwa maendeleo ya miaka ijayo.

Kiuchumi Marekani inaongoza Kwa Uchumi Kwa kiasi cha Dola Bilioni 476.5 ikufuatiwa na China Kwa Dola Bilioni 370.6 na Japan's Kwa Dola 170.5. Tafiti zinaonyesha China imewekeza sana kwenye Utafiti kama msingi wa Maendeleo; Utafiti wa Msingi asilimia 5.5%, utafiti unaotumika asilimia 10.9% na utafiti wa majaribio kwa asilimia 84%. Ni muhimu kuweka ubunifu, uvumbuzi na teknolojia kama nguzo kwa vijana katika kujenga mifumo na sera zinazojumuisha zaidi ufanisi wa kupata matokeo mazuri na endelevu katika kutimiza lengo la maendeleo katika nchi hiz (SDGs).

Hii ni wazi kwamba Kuboresha viwango na ubora wa elimu ni muhimu kuwawezesha vijana kutimiza malengo yao kwa ufanisi kwa uwezo wao wote katika Fani za Sayansi, Teknolojia, Uhandisi, na Hisabati ,(STEM) ni muhimu sio tu kwa kukidhi mahitaji ya kufanya kazi bali kwa kuzalisha watafiti na wavumbuzi wa baadaye ambao wanaweza kusaidia kutatua changamoto zinazojitokeza Tanzania na hata ulimwenguni kote kwa ujumla.

Licha ya viwango vya juu vya uandikishaji na uhitimu katika ngazi ya kimataifa, vijana hasa wanawake hawana uwezekano mkubwa wa kuzingatia masomo maalum ya STEM. Katika nchi ambazo kuna mapungufu ya kijinsia, fursa za kujitegemea, ujuzi binafsi, mawazo dhamiri, nia/nguvu thabiti hususan fursa za kiuchumi huwa ni ndogo na wanawake wanaona hamna haja ya kuchagua fani za STEM.

Pengo la kijinsia katika fani za STEM huongezeka licha ya ongezeko wa kipato zaidi bado kuna wanawake wachache kwenye fani za STEM. Sababu hazijaelezwa kikamilifu. Vile vile Ufanisi wa Wasichana katika sayansi na hisabati hauelezei mapungufu katika ngazi ya pili ya sekondari au katika soko la ajira. Kuna Sababu zinazozuia uimarishaji wa fani hizi kutoka ngazi ya mtu binafsi na jamii na kushawishi ushiriki mdogo wa wanawake katika masomo ya STEM. Hii ni pamoja na mtazamo wa mtu binafsi kwa masuala yanayohusiana na STEM, pamoja na ufanisi wa kujitegemea, uwepo wa msaada mkubwa kwenye mitandao ya kijamii, mifumo, sheria, kanuni, maadili na kanuni zinazofafanua umuhimu wa fani za STEM.

Licha ya kupiga hatua nzuri, tafiti zinaonyesha wavulana ni wengi zaidi kuliko wasichana mashuleni na yawezekana wasichana milioni 16 hawatakwenda shuleni wala darasani maisha yao yote (UNESCO Institute of Statistics). Wanawake wanahesabika kwa theluthi mbili ya watu wazima 750,000 bila ujuzi wa kusoma na kuandika. Ingawa ni kweli kwamba idadi ya wasichana wengi na wanawake wenye umri mdogo kwa sasa wanahudhuria shule kuliko hapo awali, lakini wingi wa vikwazo wanaovyokumbana navyo bado ni vingi sana, hasa kwa wasichana na wanawake katika nchi zinazoendelea

UK,10



*Phelisters Wegesa akiwa katika uwasilishaji wa Mada kuhusu Maisha na mafanikio ya Mfanyabiashara maarufu na Mkurugenzi wa Ali Baba Jack Ma Beijing China .*

ikiwemo Tanzania. Vikwazo kama mila na tamaduni potofu za kijamii, ukatili wa kijinsia, umaskini, ndoa za mapema na za kulazimishwa, mimba zisizotarajiwa, ubaguzi wa kijinsia na fikra zingine potofu ambazo ni sababu kubwa za ukosefu wa elimu kwa wanawake duniani.

Ni wazi kuwa kuna mengi ya kufanya kuboresha uwakilishi wa wanawake katika fani za STEM ambazo zimekuwa fani zinazoongozwa na wanaume. Ni njia muhimu ya kuwawezesha wanawake wawe na ujuzi na kuimarisha ujasiri wao kushiriki kikamilifu katika mchakato wa maendeleo na shughuli ambazo zinaweza kuwa na faida kubwa. Hatua za kupunguza utofauti wa jinsia ni pamoja na kuunganisha mtaala wa ubunifu (mtaala unaohusisha wanafunzi na wataalamu katika elimu ambao unahamasisha mawazo ya ubunifu na uvumbuzi) pia kuwashirikisha wavulana na wanaume katika kukuza dhamira nzuri na mabadiliko ili kujenga na kuimarisha uthubutu wa wasichana na wanawake kwa ujumla kujiunga fani za STEM.
Kuhamasisha walimu mashuleni, viongozi mbalimbali kuwasaidia wasichana na kuweka mazingira salama ya kijinsia yaliyo rafiki hivyo kupelekea kuimarisha kujiamini kwa wasichana, muhimu katika kuondoa vikwazo vya wasichana kwenye sekta ya elimu. Habari njema ni kwamba mbali na elimu ya darasani, Programu na fursa mbali mbali za ubunifu, uvumbuzi, utafiti na Teknolojia za ujasiriamali kwa ajili ya Wafanyabiashara wadogo wadogo zitasaidia wanawake kuanzisha biashara zao na kuzalisha mapato kwa kiwango cha juu na kuwa wamiliki wa biashara zao.

Tafiti zinaonyesha wanawake wanafanikiwa kwenye biashara sawa sawa na wanaume (kwa kuanza biashara, ukuaji wa mapato, kazi za kujitegemea na idadi ya miaka katika biashara). Licha ya kukabiliwa na changamoto mbalimbali kama kulea familia na upungufuwa fedha wanawake wameweza kuthubutu na wameweza. Tafiti zinaonyesha pia kuwa uwekezaji wa Elimu kwa Wanawake, umepelekea ukuaji wa uchumi kwa kasi zaidi kutoka ngazi ya familia hadi ngazi ya kitaifa kwa ujumla.

Hivyo basi ni vyema Tanzania kuundwa shirikisho la pamoja la wataalamu wanawake kote nchini ambalo kila mwaka linaweza kuleta wanawake pamoja nchini kote kujadili maendeleo, changamoto na njia ya kuziba pengo la kijinsia na huu utakuwa mwanzo mzuri wa kupata jukwaa endelevu kwa wanawakekujipambanua.Hongera Wanawake wote wanaojituma.

Mwisho kabisa ni wazi kwamba Jamhuri ya watu wa China bila shaka ni kinara wa kitaifa katika kupunguza umasikini na kuboresha matokeo na mageuzi makubwa kwenye uchumi na kuna nchi nyingi zinaweza kujifunza kutokana na uzoefu na mabadiliko ya China.

China inaendelea kuchukua nafasi ya juu zaidi kiuchumi kwa ngazi ya kimataifa na hii ni nafasi nzuri sasa mataifa mengine kushirikiana kwa karibu zaidi na nchi ya China kutokana na uzoefu wake na kuingia katika uchumi wa kisasa wa kitafiti. Mahusiano ya China na Tanzania ni muhimu sana hasa kwa vijana na hatua na mipango mikubwa imeundwa kusaidia vijana nchini Tanzania. Hatua hizi zitatoa ufadhili na mafunzo na hata nafasi za kazi na kwa ajili ya maendeleo. Kama kijana anaesoma nchini China, ni jukumu langu kufanya bora zaidi kwa kujifunza zaidi kuwashirikisha wenzangu waliopo Tanzania kuhusu fursa mbalimbali na umuhimu wa "Fani za Sayansi, Teknolojia, Uhandisi, na Hisabati kama chachu ya maendeleo endelevu. Udumu urafiki wa China na Tanzania.

Phelisters Wegesa.
Mwanafunzi jimbo la Henan nchini China
IDARA Afya ya Jamii (Public Health).

ELIMU NA UMOJA TUIJENGE TANZANIA
TANZANIA STUDENTS' ASSOCIATIONS FEDERATION IN CHINA
TASAFIC


# MIRAJI AITANGAZA VYEMA TANZANIA KIMATAIFA



*kutoka kulia ni  Samantha Sibanda muanzilishi na mkurugenzi wa "Young achievers " na wa kushoto ni H.E Ina Marciulionyte Ambassador of Lithuania wakati kati ni Mngereza Miraji baada ya kupokea  tunzo hiyo 2019 Beijing China.*

Tarehe 15.06.2019, Mtandao wa Pride of Africa Awards (POAA) ulimtaja Mtanzania, Mngereza Miraji ni mshindi wa tuzo maalum katika kipengele cha "Young achievers " iliyokuwa ikishindaniwa na Waafrika toka nchi mbalimbali ikiwemo Nigeria, Ethiopia, Cameroon,Ghana nk.  Apppreciate Africa Network ambao ni waandaaji wa tuzo za POAA umemtaja Miraji kuwa ni mshindi wa tuzo hiyo kutokana na namna alivyoongoza wenzake katika kuwakusanya Watanzania zaid 3500 kupitia mitandao ya kijamii ikiwemo whatsapp na kuwapa maelezo juu ya uombaji wa udhamini wa masomo nchini China na Uturuki.

Miraji ni mwanzilishi mwenza wa Peking University African Think Tank (PATT), http://pekingafrica.com/patt/ ambalo ni jukwaa maalum linalokutanisha watafiti wa kiafrika na Wachina chini ya Center of African Studies(CAS) ya chuo kikuu cha Peking. Miraji ni mwanafunzi wa Shahada ya Uzamivu (Phd) katika chuo kikuu cha Peking  Katibu Mkuu wa shirikisho la jumuiya za wanafunzi Watanzania nchini China(TASAFIC). Hafla ya utoaji tuzo kwa washindi ilifanyika hoteli ya Grand Concordia,Beijing na kuhudhuriwa na mabalozi wa nchi mbalimbali ikiwemo Ethiopia, Cameroun na Cabo Verde.



*Wa Nne Kutoka Kulia Ni Balozi Wa Tanzania Nchini China Mh, Mbelwa Kairuki na  Wa Nne Kutoka Kushoto Ni Mkuu Karakana Ya KutengenezaNdege Aerospace University Shenyang Nchini China Wakiwa Katika Picha Ya Pamoja Na Baadhi Ya Viongozi Wa TASAFIC Baada Ya MkutanoMKuu Nchini China  2018.*

# JE TUNAJIFUNZA NINI KWENYE "INTERNATIONALIZATION POLICY"?



*Pichani Ni Wilson Anatory Bilihanyuma pamoja Na Mussa Hassan Zyuma Wakiwa Na Wanafunzi Hao Wa Sekondari Katika Eneo Maarufu la Utarii Lijulikananlo Kama 'Movie Site – Songchen' Walipokuwa kwenye Ziara ya Kimasomo mjini Hangzhou nchini China.*

Na : Wilson Anatory Bilihanyuma

***Makala hii ni maalumu kwa watunga sera, wadau wa elimu, watu walio katika ngazi za maamzi na watu wote wanaoweza kuhusika kwa namna moja au nyingine.***

Moja ya vitu vinavyoibeba China hata kufikia mafanikio waliyonayo leo, ni uwezo wa kupanga malengo ya miaka mingi ijayo (Hadi miaka 100), kuweka malengo katika maandishi, kushirikishana malengo pamoja na kuyatekeleza kama yalivyoazimiwa. Kutokana na mipango inayotekelezeka na iliyo wazi kwa kila mtu, uwezekano wa wao kuvuka malengo waliyojiwekea huwa mkubwa kuliko kutofikia malengo. Nikiwa katika ziara ya kimasomo, niliwahi kuhudhuria hadhara moja katika chuo kikuu cha 'Zhejiang Normal University' kilichopo katika mji wa Jinhua, nchini China. Iliwasilishwa mada moja juu ya Internationalization policy. Kwa Kiswahili kisicho rasmi sana naweza kuita sera ya kuifanya China na raia wake kuwa wa kimataifa.

Sera hii inalenga kuleta mageuzi makubwa nchini China kwa kubadilisha mitazamo na tabia za watu wao kuwa za kimataifa. Wanataka kuhakikisha kwamba kila mchina ana fikra zinazovuka mipaka ya nchi badala ya kuwa na watu wenye mawazo yanayoishia palepale walipo.

Hili linakuja kutokana na msukumo usioepukika wa utandawazi ambapo ushindani wa fursa mbalimbali unazidi kuongezeka baina ya nchi moja na zingine. Lakini pia, ni kuhakikisha nchi yao inanufaika na ushirikiano wa kimataifa unaosisitizwa kwa nchi zote kuwa nao. Hivyo, wanalazimika kuandaa watu wao watakaoweza kushindana kikamilifu katika fursa mbalimbali duniani kote kupitia taasisi za elimu na mikakati mingine.

Sera hii tayari imeshaanza kutekelezwa. Hadhara hiyo, ilijikita kuelezea juhudi binafsi zinazofanywa na chuo cha Zhejiang katika kutekeleza Internationalization policy ndani ya chuo. Yafuatayo ni maeneo machache yanayofanyiwa kazi;

Kuwafanya wafanyakazi wa chuo kuwa wa kimataifa.Hili linafanyika kwa njia kuu mbili. Moja ni kuajiri wafanyakazi au wataalamu wa kigeni toka nchi zingine. Pili, ni kwa kuwaendeleza wafanyakazi raia wa China kwa mafunzo mbalimbali ya kuwafungua akili juu ya mabadiliko yanayotokea ulimwenguni kote. Lengo ni kuwafanya kuwa 'Inernationalized.'

Kuwafanya wafunzi wa chuo kuwa wa kimataifa.Hili nalo hufanyika kwa njia kuu tatu. Moja ni kuhamasisha wanafunzi wanaotoka familiza zenye uwezo kiuchumi kwenda kusoma nje ya nchi hasa kozi za lugha, utamaduni nk au hata kutembelea nchi hizo kupitia utarii, mafunzo ya muda mfupi, semina na makongamano.

Njia ya pili ni serikali kutoa ufadhiri wa masomo kwa wanafaunzi wao wanaoonekana kuwa na uwezo mkubwa darasani na wasio na uwezo kwenda kusoma nje ya nchi. Mwisho ni kupitia mpango wa kubadilishana wanafunzi baina ya chuo hicho na vyuo vingine katika nchi mbalimbali. Mfano, unasoma miaka 2 katika chuo cha nchi yako kisha unahamia chuo cha nchi nyingine kwenda kumalizia miaka miwili mingine; wanafunzi wa chuo kile unachohamia wanahamishiwa katika chuo ulichotoka nchini mwako.

Kufanya tafiti za chuo kuwa za kimataifa.Hili hufanyika kwa kuandaa mikutano ya kitaaluma ya kimataifa, kuchapicha tafiti zao katika 'Jounal' zenye ubora wa kimataifa, Kushirikiana na vyuo vya nchi zingine katika kufanya tafiti za pamoja, Kuwawezesha wanafunzi kushiriki mashindano ya kimataifa.

Kuweka mandhari au mazingira ya kimataifa katika chuo chao.Lengo hili ni kwaajili ya kuwafanya wanafunzi na wafanyakazi wote kuona mazingira ya kimataifa katika maisha yao ya

kila siku chuoni. Ilielezwa kwamba, kuna mpango wa kuanzisha kozi za Kiafrika (African studies) katika chuo hicho. Alifafanua kwamba, kozi hizo zitawawezesha wachina na watu wengine kusoma masuala mengi yanayoihusu Afrika ikiwemo Sera za nchi hasa zile zinazohusiana na Biashara, uhusiano wa kimataifa, elimu, tamaduni za kiafrika na fursa zilizopo katika bara la Afrika.

Kuwafanya viongozi wa taasisi na idara mbalimbali kuwa wa kimataifa. Katika kutekeleza hili, kila kiongozi analazimika kuwa na angalau miezi kuanzia mitatu na kuendelea ya kwenda kufanya kazi katika chuo au taasisi nyingine iliyo nje ya nchi. Lengo ni kujifunza mifumo ya utendaji maofsini na kujifunza mbinu mpya za uongozi katika nchi zingine. Wanaamini kwamba huwezi kubadili wanafunzi/rasilimaliwatu kuwa ya kimataifa bila kuwa na viongozi wenye sifa na mitazamo ya kimataifa. 'Internationalization of Institutional leaders'

Muwasilishaji alimalizia kwa kutoa mifano ya takwimu za utekelezaji za mwaka 2018 kama ifuatavyo;

•Zaidi ya theluthi moja ya wafanyakazi wa chuo walipata uzoefu wa kimataifa kuanzia miezi sita na kuendelea. Hii ilihusisha mafunzo, kufanya kazi nje ya nchi, makongamano ya kitaaluma nk.

•Zaidi ya wafanyakazi wahadhiri 100 kutoka nchi mbalimbali tayari wameajiriwa chuoni hapo. Hawa ni wale wenye shahada ya uzamivu (phd) na kuendelea.

•Wanafunzi zaidi ya 700 tayari wamepelekwa na chuo kusoma katika nchi mbalimbali.

•Wameanzisha kozi 13 za shahada ya kwanza na kozi 10 za shahada ya uzamili na uzamivu zinazofundishwa kwa lugha ya kiingereza. Ikumbukwe kwamba lugha kuu ya kufundishia nchini china ni Kichina kuanzia shule za msingi hadi vyuo vikuu.

•Wameungana na vyuo vinne toka Nchi mbali mbali kwa ajili ya kubadilishana wanafunzi na uzoefu.

Kwa maelezo yote hayo japo kwa uchache, narudia swali langu nililoanza nalo; Je, kuna cha kujifunza juu ya Internationalization Policy?

Ukikubali_Wajibu_Timiza_Wajibu!

*Wilson Anatory Bilihanyuma*
*Northeast Normal University*
*Jumuiya ya TASAJI – Jilin*
*wilsonanatory@gmail.com*

## UANACHAMA

**6. Jumuiya kuwa Mwanachama**

**6-(1)**. Jumuiya ya Wanafunzi Watanzania walio katika mji au jimbo lolote katika Jamhuri
ya watu wa China inapaswa kuwa mwanachama wa Shirikisho.

**(2)** Ili kutambulika kuwa mwanachama wa Shirikisho, Jumuiya italazimika kuwa na idadi ya wanachama wasiopungua watatu.

**(3)** Endapo Jumuiya haitafikisha idadi ya wanachama watatu, Jumuiya hiyo italazimika kujiunga na jumuiya nyengine ya jimbo la jirani.

**7. Jumuiya hai**

Jumuiya itatambulika kuwa jumuiya hai kwa kuchangia ada, michango na kushiriki shughuli
mbalimbali za Shirikisho kama ilivyoainishwa katika Kanuni hizi.

**8. Ada ya mwanachama**

Mwanachama atatakiwa kuchangia kiasi cha fedha kitakachoainishwa na jumuiya yake kwa
ajili ya mfuko wa dharura.

**9. Maombi ya Jumuiya kuwa mwanachama**

Ili kujiunga na Shirikisho, jumuiya husika itawasilisha ombi lake kwa Kamati Tendaji kwa
njia ya maandishi na Kamati Tendaji itatoa maamuzi ndani ya muda usiozidi siku 5 za kazi
baada ya siku ya kupokea maombi.

**10. Haki za jumuiya**

10.-(1) Kila Jumuiya mwanachama itakuwa na haki zifuatazo:-

**(a)** Kushiriki katika shughuli zote za Shirikisho kwa utaratibu utakaowekwa.

**(b)** Kushiriki kwa uhuru kutoa maoni na mapendekezo katika mikutano na mikusanyiko ya
Shirikisho kwa utaratibu utakaowekwa.

**(c)** Kushirikishwa na kupewa taarifa katika mambo
yanayogusa maslahi ya Shirikisho.

**(d)** Kupendekeza ajenda za vikao vya Shirikisho katika
mikutano ya Shirikisho.

**(e)** Kupata nyaraka za Shirikisho kwa njia ya machapisho, vipeperushi, barua pepe,
mitandao ya kijamii na njia nyengine yoyote kama hali itakavyoruhusu. 10

**(f)** Kuwakilisha Shirikisho katika mikutano itakayohitaji uwakilishi kama itakavyoamuliwa na Uongozi.

**(g)** Kuwakilisha Shirikisho katika mikutano mbalimbali itakayohitaji uwakilishi wa Shirikisho kama itakavyoamuliwa na Uongozi.

**(2)** Katika kufurahia haki hizi, Jumuiya mwanachama haitazitumia haki hizi kwa njia yoyote
ambayo itaathiri haki za Jumuiya nyengine mwanachama.

**11. Wajibu wa jumuiya**

Kila Jumuiya mwanachama wa Shirikisho hili itakuwa na wajibu ufuatao:-

**(a)** Kulinda, kuhifadhi, kutetea na kuitekeleza Kanuni hii wakati wote.

**(b)** Kulipa ada na michango mbalimbali ya Shirikisho kama itakavyoamuliwa na shirikisho
kwa mujibu wa Kanuni hii.

**(c)** Kuwa mwaminifu na kutojihusisha na matumizi mabaya ya fedha au mali yoyote ya
Shirikisho.

**(d)** Kufikisha taarifa mbalimbali za Shirikisho kwa wanachama wa Jumuiya husika kwa
wakati husika.

**(e)** Kuwahamasisha wanachama wa Jumuiya husika kushiriki shughuli mbalimbali za
Shirikisho.

**12. Ukomo wa jumuiya**

Jumuiya itakoma kuwa Jumuiya ya Shirikisho kwa mambo yafuatayo:

**(a)** Kufa kwa Jumuiya husika.

**(b)** Kuachishwa uanachama wa Shirikisho kwa uamuzi wa Mkutano Mkuu.

**(c)** Jumuiya kujitoa yenyewe kwa maandishi baada ya kutoa sababu za msingi na maamuzi
hayo kuridhiwa na Kamati Tendaji ya shirikisho.

**(d)** Jumuiya kukosa uwakilishi katika mikutano mikuu miwili mfululizo ya Shirikisho bila
ya taarifa rasmi.

**(e)** Kutokulipa ada ya uanachama kwa miezi mitano mfululizo bila ya taarifa rasmi.

**(f)** Kukiuka matakwa na masharti ya kanuni za Shirikisho.

**(g)** Kufa kwa Shirikisho.

# NILIDHANI ELIMU YA TANZANIA HAINITOSHI




*Pichani ni Wilson Anatory Bilihanyuma akiwasilisha mada juu ya mfumo wa Elimu ya Tanzania kwa wanafunzi wenzake darasani chuoni 'Northeast Normal University' - China*

**Na : Wilson Anatory Bilihanyuma**

Ndoto yangu ya kusoma nje ya nchi ilianza baada ya kuhitimu masomo ya shahada ya kwanza katika chuo kikuu kishiriki cha Elimu cha Dar es Salaam (DUCE). Nikiwa Chuoni hapo, nilibahatika kujifunza kozi fupi fupi juu ya stadi za maisha kwa kutumia muda wangu wa ziada. Hapo nilijifunza kanuni nyingi za mafanikio maishani zilizopelekea kuwa na maswali mengi kichwani yaliyonijengea shauku ya kusoma nje ya nchi ili kupata majibu yake.

Pia, nilikatishwa tamaa kutokana na kauli za watu za jumla kwamba elimu yetu haina ubora unaostahili. Nilijenga hofu kwamba huenda elimu ya Tanzania hainitoshi. Kwahiyo, msingi mkubwa wa maswali yangu ulitokana na hoja ya kutaka kujilinganisha na wasomi wengine duniani wenye kiwango cha elimu kama nilichofikia.

Pamoja na kwamba nilihitimu na matokeo mazuri, sikujua namna ya kuyatafsiri nje ya mipaka ya Tanzania. Nilitamani kujilinganisha kwakuwa niliaminishwa kwamba, ili ufanikiwe ni lazima ujitambue wewe ni nani na uwezo wako ni upi unaokutofautisha na watu wengine. Baadhi ya maswali yangu yalikuwa kama ifuatavyo;-

Kwanza,Nimefaulu vizuri Tanzania, nini kinanifananisha au kunitofautisha na mhitimu wa nchi nyingine wa ngazi yangu ya elimu?

Pili,Je, nina uwezo au ubora kiasi gani wa kufanya kazi nje ya mipaka ya Tanzania?

Tatu,Je, ninaweza kufanya kazi na watu wa mataifa mengine bila kuathiri tofauti za tamaduni, tabia, mitazamo, imani nk?

Pamoja na uchumi duni wa familia yangu, haikunizuia kuweka nia ya kusoma nje ya nchi. Nilijiandaa kutumia fursa yoyote itakayojitokeza mbele yangu. Kwa sababu hiyo, sikuamua nchi gani ya kwenda kusoma. Isingekuwa rahisi kwangu kuchagua nchi, wakati ninategemea ufadhiri toka kwa watu wengine. Shida yangu ilikuwa kuvuka mipaka ya Tanzania kwenda kusoma nchi yoyote au bara lolote ilimradi tu kuwe na amani na usalama wa maisha.

HATIMAYE NIKAPATA UFADHIRI WA MASOMO NCHINI CHINA

Hapa ndipo nilianza kuamini usemi kwamba "Vile unavyojifikiria wewe ndivyo utakavyokuwa". Nikiwa Mwalimu katika shule ya Sekondari Kilakala – Morogoro, Serikali ya Tanzania kwa kushirikiana na China ilianzisha somo la kichina kwa baadhi ya shule za Tanzania ikiwemo shule yangu Kilakala Sekondari.

Tuliletewa walimu kutoka China kwajili ya kufundisha somo hilo kwa wanafunzi na walimu waliopenda kujifunza lugha hiyo. Walimu hao wa Kichina, ndio sababu kuu ya mimi kupata ufadhiri wa masomo nchini China.

Waliniongoza na kushirikiana nami katika hatua zote za kuomba ufadhiri na hatimaye nikakubaliwa kufadhiriwa na serikali ya China, kulipia gharama zote kwa muda wa miaka miwili nikisoma shahada ya pili ya Uongozi katika Elimu (Master of Education Management).

Nilifurahi zaidi kupata fursa ya kusoma nchini China kutokana na sifa ya nchi hiyo kiuchumi, kiteknolojia na kisiasa. Niliamini nitajifunza mengi zaidi hata nje ya taaluma yangu. Nilipofika Chuoni, furaha yangu iliongezeka baada ya kugundua kuwa tunasoma na kuishi pamoja na wanafunzi wengine toka mataifa mbalimbali duniani. Hivyo, udadisi wangu haukuishia kujifunza kwa wachina tu, bali kwa watu kutoka kona zote za dunia. Baada ya uchunguzi wangu wa kina nilihitimisha kwa kusema, 'kujionea mwenyewe ni vizuri kuliko kusimuliwa na watu'. Watu wanakuza au kupunguza jambo kutokana na matakwa yao binafsi.

Funzo;

1. Ni vyema kutengeneza picha nzuri ya maisha yako kwa miaka mingi ijayo. Vile unavyoamini ndivyo itakavyokuwa. Usiishi bila malengo.
2. Mtu yeyote aliye karibu na wewe, ukimtumia vizuri anaweza kukusaidia kwa chochote.
3. Popote uendapo, mazuri yapo na mapungufu yapo. Usikatishwe tamaa na kauli za jumla zinazotolewa na watu wanaokuzunguka. Kuna tofauti kati ya 'mimi' na 'sisi'.
4. Ukiamua unaweza kufika popote pale utakapo kwa kutumia elimu ya Tanzania. Ni kweli tofauti zipo lakini sisi sio wa mwisho duniani. Tofauti si lazima iwe hasara, pia inaweza kuwa faida. Kuna nchi nyingi sana ziko nyuma yetu.
5. Awali niliamini kwamba, ufadhiri wa masomo nje ya nchi ni kwa watoto wa familia bora tu; lakini nimeshuhudia mwenyewe kuwa China ni mfano mzuri wa nchi zinazotoa fursa kwa watu wa hali zote za kiuchumi. Hata wewe unayo nafasi kujaribu bahati yako.

*Wilson Anatory Bilihanyuma*
*Northeast Normal University*
*Jumuiya ya TASAJI – Jilin*
*wilsonanatory@gmail.com*

# HAPPY BIRTHDAY TASAFIC 2019/20



*Viongozi Mbali Mbali Wa Tasafic Pamoja Na Wanachama Baada Ya Mkutano Mkuu Uliofanyika Shenyang, Liaoning. 1- Desemba-2018*

Na : Wilson Anatory Bilihanyuma

***Kwa mara ya kwanza, Dunia nzima itasafishwa siku ambayo kila mtu ataamua kufagia eneo lake alilosimamia "Happy birthday TASAFIC"***

Katika kitabu chake cha 'The 27 Challenges Managers face'; Bruce Tulgan anatueleza changamoto mbalimbali wanazokumbana nazo viongozi. Baadhi ya changamoto hizo zinaweza kutokana na hali ya kuwa kiongozi mpya katika taasisi husika; hali ya kupandishwa daraja kutoka mtendaji wa kawaida hadi kuwa kiongozi wa watendaji uliokuwa nao ngazi za chini; Hali ya kutokuwa na ufahamu sana wa majukumu yako, Hali ya kuwa na mtendaji aliye chini yako mwenye uelewa zaidi kuliko wewe, Tabia zisizofaa na ngumu kurekebishika miongoni mwa unaowaongoza; pamoja na Nguvu ya msukumo inayotoka nje ya taasisi unayoiongoza (External forces).
Yote hayo ni sehemu ya Changamoto zisizokwepeka kwa mzaliwa wetu mpya. Happy birthday TASAFIC.

Sina shaka kabisa na mzaliwa wetu kwakuwa amezaliwa mjini. Kule kwetu Wazaramo huwa wanasema, ukizaliwa Dar es Salaam tayari wewe ni 'Form Six'. Kwakuwa wewe umezaliwa Beijing, kwa mamlaka niliyopewa nakutunuku Shahada ya Chuo Kikuu moja kwa moja. Kuwa haraka na uwatumike wana TASAFIC wote walioonesha imani kwako hadi kukuzaa kupitia sanduku la Kura June 15, 2019. Kumbuka una mwaka mmoja tu kukua na kutumikia wana TASAFIC.

Mwanetu zingatia hili, katika changamoto zilizoainishwa hapo juu nakutahadharisha na moja wapo kubwa zaidi. Nayo ni Changamoto ya nguvu ya msukumo toka nje ya Taasisi yako (External forces). Naizungumza hii kwakuwa ni ngumu kuitabiri, ngumu kuizuia na ngumu kuitatua.

Ni hatari kwako na kwa umoja wote wa TASAFIC.
Kule kwetu kuna kabila moja ambalo mwanamke asiyepigwa na mme wake humwonea wivu yule anayepokea kipigo kila siku toka kwa mme wake. Hao ni binadamu usishangae; Hawaeleweki kabisa. Yani unakaa na mtu ukidhani unamfurahisha kwa kutompiga lakini yeye anakutafsiri kama mtu usiyejua kutunza mke kwa kumnyima kipigo anachotaka. Sababu ya yote haya sio Mume wala Mke bali ni nguvu ya msukumo toka nje ya taasisi ya ndoa yao. Nguvu hii inayotokana na itikadi au tamaduni zilizoanzishwa na mtu ambaye hata hajui madhara anayoendelea kusabisha kwakuwa alishafariki zamani.

Unaowaongoza TASAFIC, pia wana itikadi zao zikiwemo za kisiasa, kidini, kikabila, umimi, na mengineyo. Kuna wengine nia yao kubwa ni kumkwamisha mtu. Wengine hukosa furaha na kuugua kabisa wakiona unafanya mambo mazuri. Ogopa mtu ambaye anasema kwamba haoni faida wala hasara kuwa mwana TASAFIC.
Kanuni za kisaikolojia zinasema kwamba, kila mtu lazima atamani kuwa sehemu ya jamii yake. Wakati niko shule ya Bweni, Mwalimu wangu aliwahi kusema, ukimwona mwanafunzi mwenzako anapenda kukaa peke yake nyuma ya madarasa au vichakani; hakikisha unamtazama kila mara, huenda anataka kujinyonga.Usipokubali kubaki sehemu ya Watanzania wenzako hapa China, unataka kuwa sehemu ya umoja wan nchi gani? Happy birthday TASAFIC.

Kwa kusema yote hayo, ninawaomba wana TASAFIC wenzangu wote tutoe ushirikiano wa dhati kwa Uongozi mpya wa TASAFIC. Kila mtu akitimiza wajibu wake, hakika TASAFIC itakuwa na manufaa kwetu sote. Fagia eneo lako ili tuisafishe dunia; Timiza wajibu wako ili tuiendeleze TASAFIC.

Pia ninawapongeza wagombea wote waliojaribu na kura zao kutotosha, naamini wamewekeza kwaajili ya baadae. Maarifa waliyopata huwezi kuyakuta katika vichwa vya wale ambao hata hawakuiona fomu ya kugombea uongozi.

Aidha, ninaipongeza sana tume ya uchaguzi. Nikiwa sehemu ya tume hiyo, naiheshimisha kwa kuwataja majina wajumbe wote watano ambao ni Ndg. Benson Peter, Kulwa Gamba, Nicas Benard, Ummy Mohamed na Wilson Anatory Bilihanyuma. Hakika wamefanya kazi nzuri ya mfano pamoja na changamoto nyingi zilizokuwepo.

Pongezi hizi pia ziifikie kamati tendaji ya TASAFIC iliyoona kwamba tume hii inafaa kuendesha zoezi hili lililopelekea kuzaliwa kwa TASAFIC mpya. Happy birthday TASAFIC.Tuna imani na uongozi mpya wa Tasafic, tunaahidi ushirikiano wa kutosha. Happy birthday again TASAFIC; Age with Grace!

*Wilson Anatory Bilihanyuma*
*Northeast Normal University*
*Jumuiya ya TASAJI – Jilin*
*wilsonanatory@gmail.com*



Mh, Mbelwa Kairuki
Balozi Wa Tanzania Nchini China.







Phelisters Wegesa.
Mwanafunzi jimbo la Henan nchini China
IDARA Afya ya Jamii (Public Health).



Fatma Rembo.
Shahada ya uzamili sayansi ya kompyuta na teknolojia ( Uhandisi wa program)
Wenzhou, Zhejiang, China.
Wenzhou University.



Wilson Anatory Bilihanyuma
Master Of Educational Management
Northeast Normal University
wilsonanatory@gmail.coms

MSANIFU
MOHAMED MBARAKA SHAALI
ahmadishaali@gmail.com
+8615657123291

TANZANIA

# Tanzania Students

# TASAFIC

TOLEO NO.001 01/ 07/ 2019







18


Email: tasafic@yahoo.com Tell: +8615652631291 Facebook: Tasafic China Instagram: tasafic